# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE
# (2005 HADI 2015)

*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya Kongwa,*
*S.L.P. 57,*
*KONGWA*

*Mei, 2015*

# TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE WILAYANI KONGWA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2005/6– 2014/15

## UTANGULIZI

Wilaya ya Kongwa ni miongoni mwa wilaya saba **(7)** za mkoa wa Dodoma, ilianzishwa mwaka 1996 chini ya sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kifungu Na. 8 na Na. 9. Wilaya ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba **4,041** ambapo eneo linalofaa kwa kilimo na ufugaji ni hekta **363,690**. Wilaya ina Tarafa **3** za Kongwa, Mlali na Zoissa, Kata **22**, Vijiji **87**,Vitongoji **383** na Mamlaka za miji midogo miwili ya Kongwa na Kibaigwa. Wilaya imepakana na Wilaya ya Chamwino upande wa Magharibi; Wilaya ya Gairo (Mkoa wa Morogoro), upande wa Mashariki; Wilaya ya Mpwapwa upande wa Kusini na kwa upande wa Kaskazini kuna Wilaya ya Kiteto (Mkoa wa Manyara).

Kwa mujibu wa sensa ya Watu na Makazi ya mwaka **2012** Wilaya ina ongezeko la watu laasilimia **2.4;** Hivyo kwa mwaka **2015** wilaya ya Kongwa inakadiriwa kuwa na jumla ya watu **332,831** ambapo wanaume ni **160,225** na wanawake ni **172,606.** Aidha, Idadi ya kaya zilizopo kwa sasa ni **61,994**. Kaya zinazojihusisha na shughuli za kilimo pamoja na ufugaji ni **55,573** sawa na **90%.**

## MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMUYA NNE KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2005/6 HADI 2015/16

### 1. SEKTA YA UJENZI /BARABARA

- Mtandao wa barabara ya lami umeongezeka toka kilomita **60** mwaka 2005 hadi kufikia kilomita **65** mwaka 2015; ikiwa ni ongezeko la **8.3%.**
- Wilaya ina mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita **1,485;** kati yake kilomita **1,224** zinahudumiwa na wilaya na kilomita **261** zinahudumiwa na Wakala wa barabara (TANROADS).



*Sehemu ya barabara ya Suguta-Kibaigwa (km 15) ambayo inafanyiwa matengenezo*

## 2. SEKTA YA AFYA

- Wilaya ina hospitali **(1)** ya wilaya na vituo vya afya **(4)** na zahanati **53** (**45** za serikali na **8** za binafsi), hivyo kuna jumla ya vituo **58**vya kutolea huduma.
- Zahanati za serikali zinazotoa huduma zimeongezeka kutoka **27** mwaka 2005 hadi **45** mwaka **2015**.
- Aidha, zahanati nyingine **12** ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi na zitapokamilika kutakuwa na zahanati **57** za serikali sawa na **65%** ya vijiji vyenye Zahanati kati ya vijiji vyote **87.**
- Vituo vya afya vimeongezeka toka **3** (2005) hadi **4** mwaka 2015.
- Kuna nyumba **9** za wataalamu wa afya.
- Vituo vya kutoa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI (CTCs) vimeongezeka toka vituo vitano (**5**) mwaka 2005 hadi tisa (**9**) mwaka 2015; sawa na ongezeko la **80%.** Vituo vipya vinne (**4**) vimepata usajili mwaka **2014**lakini bado havijaanza kutoa huduma kutokana na kukosekana kwa samani na vifaa vya maabara na upungufu wa watumishi.

- Majengo katika Hospitali ya Wilaya yameongezeka toka **7** mwaka 2005 hadi **11** mwaka 2015; hii ni sawa na ongezeko la **57%**.
- Kiwango cha maambukizi ya **VVU** kimepungua kutoka asilimia **3.1** mwaka 2005 hadi asilimia **2.7** mwaka 2015.
- Wanachama wa **CHF** wameongezeka toka kaya **336** mwaka **2007** hadi **19,000** mwaka **2015**
- Wanachama wa **NHIF**wameongezeka kutoka **888** na wategemezi **3,704** mwaka 2005 hadi wananchama **1,871** na wategemezi **9,355** mwaka **2015**
- Vifo vya akinamama vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka **158/100,000** mwaka 2005 hadi vifo **71/100,000** mwaka 2015 ukilinganisha na **454/100,000** ya Kitaifa.
- Vifo vya watoto chini ya miaka **5** vimepungua kutoka **114/1000** mwaka 2005 hadi **6/1000** mwaka 2015; Kitaifa vifo vya watoto chini ya miaka **5**ni **154/1000**.



*Jengo la wodi 'Grade A'lililopo katika Hospitali ya Wilaya linavyoonekanakwa ndani na nje*

## 3. SEKTA YA KILIMO NA USHIRIKA

- Bajeti ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo imeongezeka kutoka Tshs. **34** milioni mwaka 2005 hadi **Tshs.848** milioni mwaka 2014/15; sawa na ongezeko la **2,394%.**
- Eneo linalolimwa mazao ya biashara limeongezeka kutoka hekta **12,832** mwaka 2005 hadi **31,515.75** mwaka 2014/15 ongezeko hili ni sawa na **145%**.
- Eneo linalolimwa mazao mbalimbali ya chakula limeongezeka kutoka hekta **83,689** mwaka 2005 hadi **94,300.5** mwaka 2014/15 ongezeko hili ni sawa na **44%.**
- Uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula umeongezeka kutoka tani **104,836** mwaka 2005 hadi tani **161,746** mwaka 2014/15; sawa na ongezeko la **52%.**
- Uzalishaji wa mazao mbalimbali ya biashara umeongezeka kutoka tani **7,565** mwaka 2005 hadi tani **16,179** mwaka 2014/15; sawa na ongezeko la **113.8%.**
- Matumizi ya mbolea(samadi) yameongezeka kutoka tani **25,335** mwaka 2005/06 hadi tani **48,500** mwaka 2014/15; sawa na ongezeko la **91%.**
- Matumizi ya wanyamakazi (Maksai) katika kilimo yameongezeka kutoka jozi za maksai **3,200** mwaka 2005 hadi **4,406** mwaka 2014/15**(37%).**
- Matumizi ya matrekta madogo (Power tiller) yameongezeka kutoka 2 mwaka 2005 hadi **26** mwaka 2014/15.
- Matumizi ya matrekta makubwa yameongezeka kutoka matrekta **314** mwaka 2005/06 hadi matrekta **685** mwaka 2014/15, sawa na ongezeko la **123.6%.**
- Kilimo cha umwagiliaji kimeongezeka kutoka hekta **178** (Tubugwe juu, Chamkoroma, Mseta na Banyibanyi) mwaka 2005 hadi hekta **487** (Tubugwe juu, Chamkoroma, Mseta, Banyibanyi) mwaka 2014/15, Hili ni ongezeko la asilimia **173.5%**.
- Maghala ya serikali za vijiji yameongezeka toka **13** (2005) hadi **25** (2014/15) wakati huo huo maghala ya watu binafsi yamefikia **194**

## 4. SEKTA YA MAJI

Katika sekta ya maji, Wilaya imepiga hatua na kupata mafanikio yafuatayo:

- Miradi ya visima virefu, visima vifupi na maji ya mtiririko inayofanya kazi imeongezeka toka **34**mwaka 2005 hadi **54** mwaka 2015 sawa naongezeko la **59%**.
- Pia Wilaya ina miradi miwili ya watu binafsi **(Kibaigwa na Ngomai)** inayotoa huduma kwa wananchi, hii ikiwa ni mkakati wa kuishirikisha sekta binafsi **(PPP)** katika utoaji huduma za jamii.
- Idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi vijijini umbali wa mita **400** imeongezeka kutoka **113,036** mwaka 2005 hadi **167,336**(52%) mwaka 2014/15; ikiwa ni ongezeko la **48%.**
- Kiasi cha wananchi wanaopata huduma kinatarajiwa kuongezeka kufikia **234,843** sawa na **72%** baada ya kukamilika kwa miradi kumi (**10**) ya awamu ya pili inayoendelea kujengwa katika vijiji vya **Mkoka, Mlanje, Pembamoto, Mlali Bondeni, Mseta Bondeni, Mlali Iyegu, Nghumbi, Chigwingili, Songambele na Ibwaga** inayofadhiliwa na Benki ya Dunia na mradi mmoja wa **Norini** unaofadhiliwa na Umoja wa nchi za Ulaya (European Union).



*Majaribio ya msukumo wa maji katika mradi wa Mlali Iyegu, ikiwa ni mmoja kati ya miradi 10 inayotekelezwa.*

## 5. SEKTA YA MIFUGO

Hadi kufikia mwaka 2014 wilaya ilikuwa na Ng'ombe wapatao **121,008**; kati yake wa kisasa ni **6,879** na wa kienyeji ni **114,129**; Mbuzi **76,724** na Kuku **414,965.**

- Majosho yameongezeka kutoka **6** mwaka 2005 hadi **23**mwaka 2014/15.
- Wataalam wa uhimilishaji (Artificial Insermination) wameongezeka kutoka **0** mwaka 2005 hadi **3** mwaka 2014/15.
- Madume bora yameongezeka kutoka **0** mwaka 2005 hadi **18** mwaka 2014/15.
- Elimu kupitia mashamba darasa ya ufugaji imeongezeka kutoka **25** mwaka 2005 hadi mashamba darasa **187** mwaka 2014/15.
- Malambo ya maji ya kunyweshea mifugo yameongezeka kutoka **7** mwaka 2005 hadi **24** mwaka 2014/15 ingawa **16** hayafanyi kazi kutokana na uchakavu wa miundombinu ya maji kuharibika mara kwa mara.
- Machinjio za kisasazimeongezeka toka **2** mwaka 2005 hadi **5** mwaka 2015 (Kongwa, NARCO, Kibaigwa,Mbande na Mkoka ambayo iko hatua za mwisho za ujenzi).
- Mabucha ya kisasa **2** yamejengwa katika miji ya Kongwa na Mbande.



*Shughuli za uchinjaji zikiendelea katika machinjio ya Mbande*

## 6. SEKTA YA ELIMU

### 6.1 ELIMU YA AWALI

- Shule za awali zimeongezeka kutoka **65** mwaka **2005** hadi **105** mwaka **2014/15;** hii ni sawa na ongezeko la **51.5%.**
- Aidha, uandikishwaji wa darasa la awali kwa mwaka **2014** ni wanafunzi **8,690**; kati yao wavulana ni **4,101** na wasichana ni **4,589.**

### 6.2 ELIMU YA MSINGI

- Shule za Msingi zimeongezeka kutoka shule **80** mwaka **2005** hadi kufikia shule **107** mwaka **2015**; ikiwa ni ongezeko la **33.8% (**shule mbili **2**ni za binafsi).
- Aidha, uandikishaji umeongezeka kutoka wanafunzi **5,674** mwaka 2005 hadi kufikia wanafunzi **10,049** mwaka 2014; hili ni ongezeko la **77.1%.**
- Idadi ya wanafunzi wa darasa la I – VII imeongezeka toka **40,473** mwaka 2005 hadi **70,291** mwaka 2015; sawa ongezeko la **74%.**
- Idadi ya walimu imeongezeka toka **830** mwaka 2005 hadi **1,174** mwaka 2015; sawa na ongezeko la **41.4%.**
- Vyumba vya madarasa vimeongezeka toka **497** mwaka 2005 hadi **656** mwaka 2015 sawa na ongezeko la **32%**
- Idadi ya nyumba za walimu imeongezeka kutoka **81** mwaka 2005 hadi **180** mwaka 2015; ikiwa ni ongezeko la **122%.**
- Uwiano wa Kitabu kwa mwanafunzi  (BPR) ni **1:5**



*Jengo la darasa na samani zake, Shule ya Msingi Mkoka (Kitengocha watoto wenye mahitaji Maalum)*

### 6.3 ELIMU YA SEKONDARI

- Idadi ya shule imeongezeka kutoka **6** (**3** za binafsi) mwaka 2005 hadi **30** (**4** za binafsi) mwaka 2015 (sawa naongezeko la **400%**). Shule mbili **(2)** za **Ndurugumi** na**Banyibanyi** ziko katika hatua za mwisho za usajili.
- Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka **1,324** mwaka **2005** hadi kufikia **6,096** mwaka **2014**; hii ni sawa na ongezeko la **360.4%.**
- Idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuingia kidato cha kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi **1,324**mwaka 2005 hadi wanafunzi **2,091** mwaka 2014; ikiwa ni ongezeko la **57.9%.**
- Shule za Sekondari za Serikali za bweni zenye kidato cha tano na sita zimeongezeka kutoka sifuri **(0)** mwaka 2005 hadi moja **(1)** mwaka 2014.
- Majengo ya kudumu ya maabara katika shule za sekondari yameongezeka kutoka 3 hadi 10 yaliyokamilika (Zoissa - vyumba **2**, Kongwa –vyumba **3**, Kibaigwa - vyumba **2,** Ndalibo- chumba **1,** Ibwaga–chumba **1** na Mlali - chumba **1).** Na mengine **68** yako hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, shule **14** zina maabara zinazohamishika (Mobile

Laboratories) na Shule nne **(4)** zimetenga madarasa ambayo yanatumika kama vyumba vya sayansi. Adha vyumba **68** vya maabara viko katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo unatarajiwa kuwa vimekamilika  ifikapo june 2015.



*Muonekanowa bweni la wavulana kwa nje na ndani, Shule ya Sekondari Kongwa*

- Majengo ya Utawala yameongezeka toka **2** mwaka 2005 hadi **8** mwaka 2015.
- Hostel za wanafunzi za serikali zimeongezeka toka **0** mwaka 2005 hadi **2** mwaka **2015.**
- Nyumba za walimu zimeongezeka toka **11** mwaka 2005 hadi **66** mwaka 2015.sawa na **500%**

## 6.4 ELIMU YA UFUNDI

- Kwa kushirikiana na Mheshimiwa mkuu wa Mkoa, uongozi wa Wilaya umeshawishi na kukubaliana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kujenga Chuo cha Ufundi Kongwa na tayari ekari  **500** eneo la **Morisheni** zimetengwa na michoro ya mipango miji imepitishwa ngazi ya Wizara  na taratibu za upitishaji wa ramani za upimaji (Survey) upo katika ngazi ya mkoa. Chuo hiki kitaweza kutoa elimu ya ufundi kwa vijana na kinakadiriwa kudahili wanafunzi kati ya **2,000** hadi **3,000** kitakapokuwa kimekamilika.
- Aidha, Chuo cha maji tawi la Dar es Salaam (Water Development and Management Institute-**WDMI**) kimetengewa ekari **100** eneo la **Chimlata** (michoro ya mipango miji

imepelekwa wizarani),ili kujenga tawi la chuo hicho kwa ajili ya mafunzo mbalimbali katika nyanja za maji na umwagiliaji. Hii nayo ni fursa itakayowawezesha vijana wengi kujiendeleza katika mafunzo mbalimbali kupitia chuo hiki.

## 7. SEKTA YA NISHATI

- Mwaka 2005 Wilaya ya Kongwa ilikuwa naumeme wa gridi ya taifa katika miji midogo ya **Kibaigwa**, **Mlali, Kongwa, Mbande,Pandambili** na kijiji cha **Mtanana**.
- Hadi mwaka 2015 jumla ya vijiji **60** (**68%)** kati ya vijiji **87** vimepata nishati ya umeme kupitia programu ya **MCC**,Vijiji (**18);** mradi wa **REA** vijiji (**38)** viko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa usambazaji umeme.Aidha, **Mh**. **Job Y. Ndugai (MB)** na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Kampuni ya **ELEKTRO MERL** toka Uholanzi inasambaza umeme jua (Solar Power) katika vijiji vinne**(4)** vya ***Ngutoto, Leganga, Silale*** *na* ***Lobilo*** na tayari ujenzi wa miundombinu katika vijiji hivyo uko katika hatua za mwisho. Hivyo kwa ujumla vijiji **66** (sawa na **75%**) kati ya vijiji vyote na miji miwili **(2)** vitakuwa vina huduma ya nishati ya umeme katika wilaya ya Kongwa mwaka huu wa **2015**.



*Ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme jua katika kijiji cha Ngutoto-Kongwa*

## 8. UTAWALA

- Idadi ya watumishi wa afya wa kada mbalimbali imekuwa ikiongozeka kutoka **181** mwaka 2005 hadi **331** mwaka 2015 sawa na asilimia **49** ya mahitaji ya watumishi **664** wa Afya.
- Idadi ya walimu imeongezeka kutoka **45** mwaka 2005 hadi **380** (ambapo wanaume ni**230** na wanawake ni **150**) mwaka 2014; ikiwa ni ongezeko la **744%.**
- Nyumba za watumishi (Utawala) zimeongezeka toka **(1)** mwaka 2005 hadi **(16)** mwaka 2015 zikiwemo nyumba **10** zilizojengwa kupitia NHC.
- Majengo ya kudumu ya ofisi za utawala makao makuu yameongezeka toka **(1)** 2005 hadi **(3)** na jengo lingine la elimu linajengwa mwaka huu **2015.**
- Majengo ya kudumu ya Ofisi za vijiji na kata zimeongeka toka sifuri **(0)** mwaka 2005 hadi **7** mwaka 2015 (Norini, Chigwingwili, Pandambili, Mkoka, Chitego, Manungu na Iduo). Awali na hadi sasa vijiji vingi vinatumia majengo ya kupanga na mengine yakiwa ni ofisi za maghala ya vijiji.



*Baadhi ya nyumba za NHC zilizonunuliwa na Halmashauri*



*Moja kati ya nyumba tano (5) za watumishi zilizojengwa na Halmashauri*

(Lilian C. Matinga)
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KONGWA**